# Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

*(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

Mkoa wa Arusha
**Telegram: Meru**
**Simu: (+ 255) 027 297-0482**
**Faksi: (+ 255) 027 297-0483**
**Barua pepe:ded@merudc.go.tz**

HALMASHAURI YA WILAYA
MERU
DISTRICT COUNCIL

**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji(W)**
**Halmashauri ya Wilaya ya Meru**
**S.L.P 462,**
**Usa River**
**Arusha**

## TANGAZO LA ZABUNI 20.05.2019

1. Halmashauri ya Wilaya ya Meru inakusudia kutumia huduma za wakala wa kukusanya Mapato ya Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kuanzia tarehe **1Julai, 2019 hadi tarehe 30 June, 2020.**
2. Halmashauri ya Wilaya ya Meru inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni,Ushirika Taasisi auVikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria,wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo kutuma maombi yao kwa zabuni kama zilivyobainishwa hapa chini :-

**(A) UWAKALA WA USAFISHAJI WA MAZINGIRA:**

| NA. | AINA YA ZABUNI | NAMBA YA ZABUNI | ENEO LA USAFISHAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | Usafishaji wa mazingira | LGA/001/2019/2020/NC/.55/Loti 1 | Kata za Ambureni, Akheri, Sing'isi Na Poli |
| 2. | Usafishaji wa mazingira | LGA/001/2019/2020/NC/.55/Loti 2 | Mamlaka Ya Mji Mdogo Usa River, Kata za Imbaseni, Maji Ya Chai, Kikatiti, Malula na Kata ya Nkoaranga *(Kijiji cha Nshupu, Pia Kata ya Nkoanekoli Kitongoji cha kwa Mangusha* |

**(B) UWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO:**

| NA. | AINA YA ZABUNI | NAMBA YA ZABUNI | ENEO LA KUKUSANYA USHURU |
|---|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa madini ya ujenzi | LGA/001/2019/2020/NC/56/Loti.1 | Kata ya Malula |
| 2. | Ushuru wa madini ya ujenzi | LGA/001/2019/2020/NC/56/Loti.2 | Kata za Usa River,Maji ya chai,Kikwe,Maroroni,Majengo naKikatiti |
| 3. | Ushuru wa Mazao . | LGA/001/2019/2020/NC/57 | Katika maeneo yote ya Halmashauri ya Meru |

## MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

**3. Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-**

3.1 Mwombaji lazima awe na leseni hai ya biashara husika TIN, Hati ya Usajili wa jina la biashara na ofisi inayotambulika.

3.2 Mwombaji awe na uwezo wa kifedha, athibitishe kwa kuambatanisha'BankStatement'ya miezi miezi (3) mfululizo iliyopita kutoka tarehe aliyoomba zabuni au'Audited Financial Statement'ya miaka miwili ya karibuni.

3.3 Mwombaji aambatanishe **"Power of Attorney"**iliyothibitishwa na Bodi ya wakurugenzi kwa zabuni husika.

3.4 Ada ya maombi ya zabuni ni **Tshs.50,000/=** (Shilingi Elfu hamsini tu), ambapo mwombaji atatakiwa kufika Halmashauri kwa ajili ya kupewa Ankara kisha malipo yatafanyika kupitia akaunti ya Halmashauri ya Meru iliyoko katika Benki ya NMB tawi la **Clock Tower Namba ya Akaunti. 40801200330**. Pia ikumbukwe kuwa Malipo yaliyotolewa kama ada ya zabuni hayatarudishwa.

3.5 Mwombaji awe na vifaa na vitendea kazi vya kutosha kumudu vyema zabuni aliyoomba.

3.6 Mwombaji awe tayari kulipa dhamana ya zabuni ya kiwango cha **mwezi mmoja (1)** cha maoteo kwa mwezi.

3.7 Awe tayari kutumia viwango vilivyowekwa katika Sheria ndogo za Halmashauri vya ukusanyaji wa mapato.

3.8 Mzabuni atakayeteuliwa atatumia mashine za kielektroniki**(POS)** za Halmashauri kukusanyia ushuru.

3.9 Kwa Zabuni zenye **'Lot'** Mwombaji anaruhusiwa kuomba zaidi ya 'Lot' moja kwa kadri ya uwezo wake, kila 'Lot' inajitegemea.Mzabuni hataruhusiwa kuomba "Lot"zaidi ya moja kama zabuni moja, hii ina maana kuwa, ukiomba 'lot' zaidi ya moja, utatakiwa kununua makabrasha ya zabuni kulingana na zabuni unazohitaji.

3.10 Maombi yawe na maelezo ya kina na viambatisho husika (kama Company Profile, n.k).

3.11 Maombi yote yafungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri [seal], na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja aina ya zabuni, namba ya zabuni na "Lot". Zabuni hizo zipelekwe katika sanduku la zabuni lililoko katika ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya ya Meru **(Na. 37)** kwa kutumia Anuani ifuatayo:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Meru,**
**S.L.P 462,**
**Usa River.**

3.12 Maombi yatakayoletwa kwa njia ya Fax, Telefax, na Telegraphic System na yatakayochelewa Hayatapo kelewa na hayatafunguliwa siku ya ufunguzi.

3.13 Kabrasha la zabuni na maelezo pamoja na masharti mengine yanapatikana yameorodheshwa kwenye kabrasha lenye Zabuni husika litakalopatikana katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Chumba **Na.37** Ghorofa ya kwanza, kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka saa 9:30 alasiri (siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko).

3.14 Maombi ya Zabuni zote yawasilishwe katika Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni wa Halmashauri, Makao Makuu ya Halmashauri ya Meru. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni ***Jumatatu, tarehe 3/06/2019, saa nne (4) asubuhi***. Waombaji au wawakilishi wao, wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo utakaofanyika siku hiyo ya tarehe ***3/06/2019 saa nne (4) asubuhi*** katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.

Emmanuel J Mkongo
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYAA YA MERU**